

Katama G.C. Mkangi

1978 (1975)

UKIWA

Nairobi: Oxford University Press

Nacherzählt von

Lourenco Noronha

Mzee Baruti¹

Lektor (1974-2009) für Swahili-Literatur
am

Institut für Afrikawissenschaften
der Universität Wien

Taasisi ya Taaluma ya Bara la Afrika
Chuo Kikuu cha Vienna

Stand: November 2008

¹ *Ndilo jina nililolipewa shuleni Tanzania 1961-1972*

Kutabaruku
Widmung

Nawashukuru walimu wangu katika
Idara ya P.W.D., Dar es Salaam, 1950-1953
pamoja na wanafunzi wa
Forodhani (St. Joseph's) Secondary School, Dar es Salaam, 1961-1968
na
Sangu Secondary School, Mbeya, 1969-1972
walionifunulia siri (mbinu) za lugha ya Kiswahili

al-hamdu li-llahi
subhanahu wa-ta'ala

Dibaji
Vorwort

Angeregt wurden diese didaktischen Unterlagen von Studierenden am Institut für Afrikawissenschaften der Universität Wien.

Die deutschsprachigen Textteile wurden von Dr. Franz Rader korrigiert; dieser hat während seiner Tätigkeit an der Österreichischen Botschaft in Nairobi meine Berufung nach Wien gefördert. Für beides bin ich ihm dankbar.

Lourenco Noronha
Ungargasse 38/431
A-1030 Wien
E-mail: noronha@gmx.at

Dhamira Kuu
Leitgedanke

Matano (Ich-Erzähler)

„Ilikuwa nimlaumu nani?
Yeye, mimi au ulimwengu? “

Katama G.C. Mkangi
Ukiwa
Nairobi: Oxford University Press
Uk. 99

1. Einleitung
Utangulizi

1.1. Biographische Notizen
Wasifu wa Mtunzi

Katama G.C. Mkangi alihitimu ualimu katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam 1971 na baadaye alikuwa mwalimu katika Shule ya Sekondari kwao Ribe, na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Aggrey, Wundanyi. Mwaka wa 1974 alipata hati ya M.A. Chuo Kikuu cha Sussex, Uingereza, na baadaye alirejea Kenya ili kufanya uchunguzi juu ya Elimu-Jamii. Anakusudia (1975) kuipata shahada ya Ph.D. ya Chuo hicho hicho.²

1.2. Thematische Einführung
Kiini (dhamira, dhana, mada, wanda/ma-) maalum

Hii ni hadithi ya kisasa ya mapenzi. Kijana anayesomea digrii kwenye Chuo Kikuu anapata simu kuwa mpenzi wake amekufa. Hapo anaanza kurudi nyuma na kutazama maisha yao yalivyokuwa na marehemu ili aweze kuivunja kasi huzuni aliyonayo. Hadithi hii pia inaonyesha migongano inayotokana na nyendo na tabia zilizoathiriwa na Uzungu na maadili ya kiasili ya mapenzi ya ndoa ambayo mwanafunzi wa chuo kikuu na mpenzi wake asiye na elimu ya kiwango chake wanayaleta katika mapenzi yao.³

Euphrase Kezilahabi hatte in Rosa Mistika die Ansicht vertreten, daß äußere Faktoren das Leben eines Menschen entscheidend bestimmen, so wie im Falle des Mädchens Rosa Mistika. Mkangi dagegen lässt in diesem Text den Erzähler Mtano die Frage stellen: „Wem sollte ich die Schuld geben; ihr, mir selbst oder der Umgebung (dem Milieu)?“⁴ Es geht ihm um die Frage, was eigentlich Lilas Verhalten verändert hat. War es der Klassenkonflikt zwischen ihm, einem Universitätsstudenten und Lila, einem Mädchen aus dem Slum; oder „*amenaswa na maisha ya anasa*“ (uk. 101); oder war es der Einfluss Europas im Zuge der Globalisierung? Auffallend ist Lilas Aussage auf englisch in ihrem letzten Gespräch mit dem Ich-Erzähler: „Sijali. *I know what I am doing*. (Uk. 96). Der Autor ist in Kenia aufgewachsen, unterrichtete in einer Sekundarschule dort und studierte in England. In diesem Text macht er die Jugend Kenias auf unterschiedliche Verhaltensmuster aufmerksam. Der Onkel Matanos sagt z.B. „Warum soll küssen auffallen? Es gibt viele Mädchen, die du küssen kannst, ohne dich zu irgend etwas zu verpflichten. Hast du nicht Europäer gesehen, die unverbindlich küssen?“⁵ Matano antwortet: „Sie sind halt Europäer. Aber bei Afrikanern – besonders bei Mädchen – wenn es (sie) zustimmt unverbindlich geküsst zu werden, dann ist es (sie) wie billiges ‚Gemüse‘“.⁶

² Rückseite des Umschlags

³ Rückseite des Umschlags

⁴ „Ilikuwa nimlaumu nani? Yeye, mimi au ulimwengu?“ (uk. 99).

⁵ „Kwani kubusu ndiyo nini? Wako wangapi unaweza kuwabusu kisha usiume chochote? Hujapata kuona Wazungu wakibusu vivi hivi?“ (uk. 14).

⁶ „Basi hao si wazungu? Lakini kwa Mwafrika – hasa msichana – akubalipo kubusiwa kwa urahisi huonyesha ya kwamba yu ‘mboga’ tu.“ (uk. 14).

Das Wort *ukiwa*⁷ - die Überschrift des Kurzromans – spricht Lila bezogen auf den Ich-Erzähler Matano gegen Ende der Erzählung (*uk.* 98). Der Umschlag des Kurzromans trägt den Titel in Weiß auf einem schwarzen Hintergrund.

Zum Ende Lilas sagt der Ich-Erzähler: „ (...) *mbele hakuendeki na nyuma hakurudiki. Lililosalia ilikuwa yeye kutapatapa.* (*Uk.* 94). Woran Lila gestorben ist wird dem Leser nicht mitgeteilt. Man könnte den Namen Lila mit der Farbe der Sehnsucht identifizieren.

Die Sprache entspricht den Erfordernissen des *Kiswahili Sanifu (Standard Kiswahili)*. Der reiche Wortschatz, die klaren Sätze und der logische Aufbau dieses Kurzromans machen ihn für Schüler der *Secondary Schools* geeignet.

Ukiwa ist zwar der Gattung Erziehungsroman zu zurechnen, sollte aber literarisch höher gestuft werden als Salome, Sitaki, Shida und Chozi la Furaha. Der Kerngedanke ist auch anders, nämlich der Konflikt zwischen der afrikanischen Lebensweise und dem europäischen Einfluss.

1.3. Literaturhinweise *Marejeo (Marejeleo)*

Die Zahlen in Klammern beziehen sich auf die jeweilige Signatur der Fachbibliothek für Afrikawissenschaften und Orientalistik der Universität Wien.

1.3.1. Primärliteratur

- Mkangi, Katama G.C. 1975. Ukiwa. Nairobi: OUP/ EAEP. 102pp. (B.8.6.14.).
Mkangi, Katama. 1984. Mafuta. Nairobi: Heinemann/ EAEP. 92pp. (B.8.6.206.).
Mkangi, Katama. 1995. Walenisi. Nairobi: EAEP 190pp. (B.8.6.261.).

1.3.2. Sekundärliteratur

- Wamitila, Kyallo Wadi. 1997. "Reading the Kenyan Swahili Prose. A Terra Incognita in Swahili Literature", in: AAP. Köln: Institut für Afrikanistik der Universität Köln. 51, Swahili Forum IV, S. 117-125. (Z.1.26.51.).
Wamitila, Kyallo Wadi. 1998. "Towards Unlocking Katame Mkangi's *Walenisi*. A Case of Parabolic Narrative", in: Kiswahili. Dar es Salaam: TUKI. 61, S. 83-93. (Z.1.10.61.).
Wamitila, Kyallo Wadi. 1999. "Interfigural Phenomena: A Tentative Investigation into Independence of Literary Characters in Swahili", in: Swahili. Dar es Salaam: TUKI. 62, S. 81-91. (Z.1.10.62.).
Wamitila, Kyallo Wadi. 1999. "What's in a Name: Towards Onomastics in Kiswahili Literature", in: AAP. Köln: Institut für Afrikanistik der Universität Köln. 60, S. 35-44. (Z.1.26.60.).

Siehe auch die Datei Swahili-Literaturliste auf dieser Website www.swahili-literatur.at

⁷ „Nakuomba uje upate msichana mwingine ambaye atastahili mapenzi yako kuliko mimi nilivyokufanyia na kukuachia ukiwa hali bado ni hai.“ (*Uk.* 98).

2. Matini Texte

Shule ilikuwa imefungwa kwa likizo ya Pasaka. (Uk. 1)

Ich⁸ hatte zu Ostern Schulferien. Ich besuchte meine „Großtante“ (nyanya), die jüngere Schwester der Mutter meines Vaters.

Bibi alikuwa anakaa mtaa wa Spaki, katika mji wa Mombasa. Hakuwa na kazi ya kuajiriwa bali alikuwa akioka chapati na kupika wali aliokuwa akiwauzia wafanyi kazi⁹ wa hali ya chini, hasa makuli wa Kilindini. Kila jioni alikuwa akiugeuza ukumbi wa nyumba yake, ambayo sijui alijenga lini, kuwa hoteli.¹⁰ Meza moja ndefu na ubao wa kulingana ndivyo vilivyokuwa vikalio vya hoteli hiyo ya mchwara mchwara. Wanunuzi walinunua chapati na nyama, wali na matumbo, muhogo na mbaazi, au mchanganyiko wa hivi vyote. Walipakuliwa sahani na kulia vijiko ambavyo kila baada ya kutumiwa vilichovywa katika maji ya vuguvugu ambayo yoo yenyewe yalikuwa machafu. Ajabu ni kwamba hakukuwa na aliyedhurika.

Taa kubwa la kopo lililotoa mwangaza wa kutosha lilikuwa kubwa mno mpaka utambi wake ukawa si rahisi kuzimika, hata kuwe na upepo wa namna gani. Taa lenyewe lilikuwa likinywa nusu lita ya mafuta kila usiku. Kwa kweli lilikuwa taa la kopo la kipekee, nami nilikuwa kila wakati nikisema, „Wa ama nyanya anatumia ubongo kweli!“

Mtaa wa Spaki unakaa (unakaliwa na) watu kama huyu bibi. Si wote ambao walikuwa wakiuza chakula. Wengine walikuwa wakiuza tembo la mnazi, piwa ama chang'aa. (Wale) Ambao wanaangalika kidogo walikuwa ama wamewekwa kinyumba au wanaishi maisha ya kimjini. Inyeshapo mtaa mzima huwa na matope na uchafu kuanza kutoka uvundo. Mahali pengine hujaa maji na kwa muda mabata hujipatia maziwa ya kuogelea.

Nyumba ya Spaki, kama nyumba nyingine za Kiafrika, ni za udongo na zilizoezekwa kwa makuti au mabati mabovu mabovu, na kwa hivi maisha huwa ya taabu wakati wa masika. (...) Na wakati wa kiangazi vyumba havikaliki wala havilaliki kwa vuguto. Ajabu ni kwamba katika mitaa kama hii ya kienyeji ndiko ambako wasichana wengi huzaliwa na kulelewa. Mtaa huu, kama mitaa mingine ya hali ya chini, ulikuwa maarufu kwa wasichana warembo na wa kuisimua. Na, kama nyanyangu, Lila pia alikuwa mwana wa Spaki. (Uk. 1-2)

Dass gerade dieser Stadtteil wegen seiner hübschen und fröhlichen Mädchen weit herum bekannt sein sollte, kommt mir sonderbar vor. Aus diesem Bezirk stammte Lila.

Ich kam sehr früh bei meiner Großtante an. Sie war gerade dabei, das Mittagessen für ihre Kunden zu kochen. Sie begrüßte mich herzlich und wollte mehr von der Schule und von meiner Reise hierher hören. Sie sagte auch, daß es mit ihrer Gesundheit nicht gut stehe. Trotzdem wollte sie arbeiten. Auf das Rauchen von starken Zigaretten wollte sie

⁸ Auf Seite 5 erfährt der Leser, daß der Erzähler Matano heißt.

⁹ *Mfanyakazi* ist ein arbeitender Mensch und *mfanyi kazi* ist ein Arbeiter.

¹⁰ *Hoteli* bzw. *mkahawa/mi-* ist ein Restaurant und *Guest House* ein Hotel.

nicht verzichten. Sie ist etwa 55 Jahre alt. Ihr Gesicht und ihre Körpergestalt deuten darauf hin, dass sie in ihrer Jugendzeit sehr hübsch gewesen sein muss. Wenn sie hinausgeht, trägt sie ein schwarzes Kleid und ein Buibui (Baibui), so wie die Küstenfrauen, die sich zum Islam bekennen, es zu tun pflegen. Aber jetzt trug sie ihre gewöhnliche Arbeitsbekleidung. Sie brachte mir das Essen. Während ich aß, kam sie auf Lila zu sprechen, die sie als meine Freundin bezeichnete.

„Vipi rafikiyo?“

„Nani?“

„Ooo, Lila! Lila si rafiki yangu. Ama ni kwa sababu tulikuwa tukisoma upande mmoja?“ nikamuuliza. Ghafula nikaingiwa na wazo, kwa hivyo nikamuuliza, “Kweli yuko?”

“Yuko! Yuko kwa mamake. Nao pia walifunga shule majuzi tu,” alinjibu na huku akivaa buibui.

“Unakwenda wapi?”

“Dukani nika...”

“Kaniitie basi,” nikamkatisha.

Msichana aitwaye Lila kwa jina la kinyumbani, ama Tede kwa jina la Kikristo, hakuwa mgeni kwangu, wala mimi kwake. Sifa zake zililaki kabla ya yeye mwenyewe kumwona. Nilimwona lini kwanza? Ndiyo, nakumbuka. Ni mwaka wa sitini na mbili nilipomwona awali. Naikumbuka kabisa siku hiyo. Ilikuwa wakati wa masomo ya alasiri, nami nilikuwa nimetumwa na mwalimu wangu wa michezo kwenda kwao shuleni kuchukua mipira. Nilipowasili nilimwona akitoka darasani. Alichopoka tu kwa haraka sana lakini nikawahi kuona sura yake. Na kwa kuwa ilikuwa ngeni kwangu, niliuliza, “Msichana gani yule?”

“Ni Tede Lila,” nikaambiwa.

“Oooo, ni yule msichana aliyetoka mjini kuja kusomea huku?”

“Ndiyo,” nilijibiwa, nami nikatosheka.

Kati ya sisi wawili, ni yeye aliyeanza kunisemesha. Ilikuwa hivi: nilikuwa nikienda kwa matibabu, na njia ya huko inapita shuleni kwao. Nilipokuwa nikipita, nilimwona amekaa na mwenziwe wakipiga domo. Huyu mwenzake alikuwa akinifahamu, naye akatangulia kunisalimu.

“Matano hujambo?”

„Hofu kwako,“ nikamjibu.

“Nasi sasa. Unae...”

„Ala, kumbe wewe ndiye Matano?“ Lila akadakia.

„Ndiyo,“ nilimjibu kwa mshangao kidogo, na tena nikawahi kuuliza, „Kulikoni?“

„Nina salamu zako.”

“Kutoka kwa nani?”

„Kutoka kwa yule nyanya ... eeee, kule Spaki, Mombasa?“

„Aha, nyanya Binti Ali!”

“Ndiyo,” akaitika. (Uk. 4-5).

Damals besuchte Lila die letzte Volksschulklasse und ich die letzte Sekundarschulklasse. Während der folgenden vier Monate hatten wir kaum Gelegenheit miteinander zu sprechen. Jeder von uns war mit seinen eigenen Angelegenheiten beschäftigt und wir maßen unserer Bekanntschaft keine besondere Bedeutung zu. Ich

freute mich sehr, als ich vernahm, dass sie die Prüfung bestanden und die Zulassung zur Sekundarschule bekommen hatte. Auch ich hatte Glück, denn ich wurde in Form V, die Vorstufe zum Universitätsstudium, aufgenommen.

Ich hatte Sehnsucht, sie wiederzusehen. Während ich darüber nachdachte, hörte ich jemanden an der Türe klopfen. Es war Lila. Sie sagte mir, daß meine Großtante bei ihr war und ihr mitteilte, dass ich hier bin. Ich gratulierte ihr wegen ihres Erfolges bei den Prüfungen. Ich entschuldigte mich, dass ich ihrer Einladung zu Neujahr nicht Folge leisten konnte. Sie hatte zwar auf mich gewartet und hätte sich über meinen Besuch gefreut, wollte aber nicht daran erinnert werden. Wir plauderten über das Studium und über Sport. Inzwischen kam meine Großmutter von der Arbeit zurück und empfahl mir, Lila nach Hause zu bringen. Als wir bei ihr ankamen, war ihre Mutter zu Hause. Nach einem kurzen Gespräch mit Lila verabschiedete ich mich von ihr, mit der Hoffnung sie wiederzusehen.

Lilas Mutter erlaubte ihr, mich zur Bushaltestelle zu begleiten. Unser Gespräch wurde unterwegs immer persönlicher. Wir blieben stehen, umarmten und küssten einander. Sie wollte mehr von meinem Leben hören, was ich ihr auch versprach, falls sie mich am kommenden Samstag besuchte. Ich suchte dabei nach einem Anlaß, sie bei mir zu haben.

Als ich nach Hause kam, rügte mich mein Onkel, weil ich stark verspätet war. Er wohnte in einer schönen Wohnung mit zwei Schlafzimmern. In der Stube gab es eine Stereoanlage und eine Hausbibliothek. Vom Fenster der Wohnstube aus konnte man die Bushaltestelle sehen. Mein Onkel, der in der Stube saß und die Zeitung las, wollte wissen, was mich eigentlich veranlasst hatte, so spät nach Hause zu kommen. Ich berichtete von meiner Bekanntschaft mit Lila und von ihrem bevorstehenden Besuch am kommenden Samstag. Er freute sich. Er war zwar mein Onkel, aber nur drei Jahre älter als ich und hatte das gleiche Interesse eine Freundin zu haben wie ich. Er riet mir aber, vorsichtig zu sein.

Baada ya kukaa kimya kwa kiasi, alitoa kauli na huku akichekacheka, „Wazee walisema: ‚Usikate mbeleko kabla ya mtoto kuzaliwa’¹¹. „

„Unamaanisha nini hivyo?“ nikamwuliza.

„Ya kwamba unajadili mambo kutoka upande wako binafsi. Kwanza Jumamosi haijafika, huenda pengine asije! Ama yeye naye atunga siasa yake ya kuja kukuhepa.“

„Ajuaje kuhepa huyo msichana?“ nikaingilia kati. „Mtu ambaye haikunichukua hata masaa matatu kumbusu!“

„Kwani kubusu ndiyo nini? Wako wangapi unaweza kuwabusu kisha usiume chochote? Hujapata kuona Wazungu wakibusu vivi hivi?“

„Basi hao si Wazungu? Lakini kwa Mwafrika – hasa msichana – akubalipo kubusiwa kwa urahisi huonyesha ya kwamba yu ‘mboga’ tu¹²,“ nikabisha.

„Huenda ikawa, lakini wako walio tofauti.“

„Lakini huyu si mmoja wao; hiyo nina hakika,“ nikakaza. Lakini haikuchukua muda mrefu kugundua kwamba Lila alikuwa mmoja wao.

¹¹ Sprichwort. Siehe den Link [Methali](http://www.swahili-literatur.at) auf der Website www.swahili-literatur.at

¹² Redewendung

Ubishi wangu kwamba msichana anapokubali kubusiwa huwa yuko tayari kuvuliwa nguo zake haukutokana na kani tu, bali pia na mazingira niliyokulia nayo. Mazingira yenyewe yalinifunza kwamba bikira halisi haimfalii kujua vipengele vya mahaba kabla ya kuolewa, ama kama wenyewe wasemayo, “mpaka baada ya kupata nyumba¹³ yake.” Kwa hivyo haya mambo ya leo ya kubusiana, kushikana mikono, kupelekana sinema au madansi, yalikuwa marufuku kwa msichana wa tabia imara.

Jambo jengine (lingine?) ni kwamba kubusiana si kitu cha asili katika mila zetu. Ni kitu kigeni, na inawezekana kuwa babu zetu hawakujua kamwe kuwa kulikuwa na kitu kama hicho. Ugeni huo ndio uliotufanya sisi chipukizi kufulizia kutekeleza “elimu” hii mpya kwa vitendo. Kwa kutokuwa na ujuzi wa kutosha na ujasiri kamili, wengi wetu hujikuta tukibusu kwa ghafula na bila dhamiri, mwisho wala si mwanzo wa chezo za mahaba. Hivi tukakugeuza kubusiana kuwa ni kishindikizo si kianzisho cha mapenzi, kama wavumbuzi wa kubusiana walivyokusudia. Na kwa kuwa katika kukua kwangu nilikuwa sijakuta msichana aliyekubali kubusiwa hali akiwa “macho wazi”, ingawaje alikubali muda kidogo tu baadaye, nilidhania kwamba msichana yeyote yule aliyehamaki kubusiwa alikuwa kwa kweli “rahisi”. Kwa sababu hii, itaonekana kuwa kule Lila kukubali kubusiwa nami siku ile ya mwanzo wa uhusiano wetu kulinipa matumaini. Kumbe matumaini yenyewe yalikuwa kama umande wa alfajiri; punde tu yalitoweka. (Uk. 14-15).

Ich aber hoffte nur, daß der Samstag bald käme. Die ganze Woche verbrachte ich mit dieser Sehnsucht nach Lila. Als ich dann am Samstag aus dem Fenster schaute und sie aus dem Bus steigen sah, freute ich mich sehr¹⁴. Aus lauter Aufregung schien mein Verstand „kuganda“ (uk. 16) und ich schwitzte an den Handflächen, die ich an meinem Hemd trocknete. Ich ging zur Haustüre, ließ sie eintreten, bevor sie noch um Einlass bitten konnte und führte sie in die Stube.

„Ho-“, Hakumaliza kupiga hodi kwani nilikuwa nimeshafungua mlango.

„Huna haja,“ nilimkatiza, „Karibu ndani,“ nikamkarbisha.

„Asante; mbona wima wima hivi? Uliniona nikishuka nini?”

„Huenda ikawa! Vipi, je salama?”

„Sijambo, habari ya kazi?”

„Sawa tu, karibu ukae, huku nikimwelekeza kiti. (Uk. 16).

Sie saß nahe beim Fenster, von wo frische Luft fächelte und ich saß an ihrer rechten Seite. Wir konnten miteinander sprechen, ohne einander anzuschauen.

Lila alikuwa amevaa rinda lenye mistari iliyotoka juu kuelekea chini. Ijapo mistari hiyo ilikuwa ya kukahawia, rinda lenyewe lilionekana kama la kipunda milia. Urefu wake ulikomea kwenye mbinu za magoti. Hii ni kusema kwamba sehemu ndogo ya mapaji yake ilionekana alipoketi, kwani nguo ilivutika nyuma na mara kwa mara ilimpasa kujiinua kidogo na kuivuta mbele aliponifuma nikikodelea macho mapaja yake. Kwa kweli yalivutia sana.

¹³ Redewendung. *Kupata nyumba* bedeutet „heiraten“, bezogen auf eine Frau.

¹⁴ An dieser Stelle spricht der Autor den Leser an, wie es in der Oral-Literatur üblich ist: „Na kwa sababu hii ndiyo unaweza kuelewa hali niliyokuwa (niliyoikuwa) nayo ...“ (Uk. 16).

Nywele zake nyeusi zilikuwa zimevutwa nyuma na kusitiriwa na pini pana kidogo, mfano wa mwezi mchanga. Mtindo huu wa nywele uliutoa nje uso wake uliokuwa mpana kiasi, na uliokaa kama moyo. Alikuwa amebeba mkoba na fedha kiasi cha nauli ya basi. Huenda pengine mlikuwa na poda na kioo pia! Kitambaa chenyewe alikitoa punde baada ya kukaa, akajifuta jasho huku akitupa macho chumbani.

„Unakaa na nani?“ aliniuliza.

“Na bamdogo.”

“Yuko?” akauliza kwa sauti ya kuonyesha hofu.

„Ndio ... anapumzika. Wache nimwite aje akusalimu.“

„Usimsumbue, mwache alale tu,“ alinizuia.

„Usiogope, nishamweleza kwamba utakuja. Mmmm, yeye alitaka kuonana nawe; kwanza nadhani yu macho ...“ „Mzee!“ Nikamwita.

„Naam,“ akaitika.

„Mgeni ashafika,“ nikamwelza. (Uk. 17-18).

Ich stellte ihn ihr mit seinem Namen Enklete Chai vor. Er hieß sie herzlich willkommen, bat mich, ihr Getränke zu bringen, plauderte ein wenig mit ihr und ging hinaus. “Nyumba nzima ikasalia sisi wawili – kinyasi¹⁵ na mbuzi“ (uk. 20). Wir waren in der Wohnung allein. Bald darauf wollte Lila sich von mir verabschieden.

„Nataka kwenda,“ Lila alisema.

“Sasa mbona hivi?” niliuliza katika hali ya mtu anayetaka kulia.

“Nishakwambia mambo haya siyajui ...”

“Uyajue basi leo. Si kila kitu kina mwanzo wake?” nikasisitiza.

“Na wakati wake, ” akaongeza.

Wakati huu wote tulikuwa tumelala nusu uchi kitandani punde tu baada ya kutoka bamdogo. Kwanza nilidhani kazi yangu itakuwa rahisi kwa kutosita kwake nilipomwongoza chumbani kwangu. Alinitia tamaa zaidi alipojitupa mwenyewe kitandani bila ubishi kama ilivyo kawaida ya wanawake. Tabia hii yake ilivuruga kabisa vitego vyangu ambavyo nilikuwa nimeviandaa ili kumnasia. Pia sikuona ugumu wowote alipojilaza yeye mwenyewe. Nami sikuzubaa, nilifuata mkondo: nikajitupa kitandani.

Nilianza kichwani kuteremka chini ... Tuliondoa ile pini na hivi iliwezesha fundo la nywele kuchanuka. Nilitia vidole vyangu nyweleni na nikaanza kuchezecheza nazo. Hatimaye nilipitia usoni. Niliupapasa kwa uangalifu kana kwamba ulikuwa yai; kuwa ungeponyoka ungepasuka. Shingo yake ikawa daraja iliyofikisha kifua kutoka kichwani. Maziwa yalisimama wima kama kunidharau na hivi ilinibidi niyasage kwa kifua changu. Niliupitisha mkono wangu nyuma – ubavu mpaka ubavu kwani kiuno chake kilikuwa chembamba – na nikamvuta taratibu. Naye akaitikia kwa kupitisha mkono wake kwangu mabegani. Sote tukavuta pamoja na midomo ikalengana.

Niliendelea na safari yangu lakini sasa kwa kasi kidogo. Niliteremsha zipu bila idhini.

„Joto,“ nikasema.

„Sana,“ akajibu.

„Si heri tuvue hili rinda lako basi?“ Nikatoa shauri ambalo lilifuatwa bila wasiwasi.

¹⁵ Vielleicht ein Diminutiv von *nyasi*/- Elefantengras *Imperata cylindrica*

Sikutosheka, kama ile hadithi ya ngamia na Mwarabu. Lakini wakati huu “Mwarabu” hakumtimiza “ngamia” matakwa yake yote. Ngamia alisihi, akambembeleza na mwisho akatia na nguvu pia, lakini hakufanikiwa. Uchu ulimwisha na hasira zikampanda ndipo akasikia “Mwarabu” anataka kuvunja hema. Kusikia hivyo, alifanya ujasiri mwingine (mwingine?) ambao alidhania pengine huenda ukafanikiwa, lakini alikatwa ini aliposikia:

“Fanya adabu tafadhali.”

“Wan’tusi?” Hasira zikanipanda.

“Sivyo. Nakuomba tu,” alinjibu huku akinyayuka. Halafu akaongezea, „Nataka kwenda, giza laingia.”

Nilikubali kushindwa. Sikufurukuta zaidi. Tulivaa nguo zetu bila kusema. (Uk. 20-21).

Ich war voller Fragen. Ich fragte mich: „Je, si kawaida ya wasichana kusema sio kumbe wana maana ya ndio, kama Waingereza wasemayo?” (Uk. 22). Ich hatte den Eindruck, daß sie meine Fragen erriet. Sie sagte: „Najua huniamini“ und fügte hinzu: „Ngoja siku moja.“ (Uk. 22).

Auf dem Weg zur Bushaltestelle beklagte sie sich, dass Burschen schlecht über ein Mädchen reden, wenn es mit einem Jungen gesehen wird.

„Unaguna nini?” Wakati huu tulikuwa tulitoka na kuelekea stani (standi?).

„Juu ya tabia za nyinyi wavulana,” akajibu.

„Zina nini?”

„Ni za ajabu kwa kuwa kila muonapo msichana na mvulana pamoja, basi mnashuku msichana mbaya.” (Uk. 23).

Als ich ihr vorschlug, dass wir uns am folgenden Tag treffen sollten, lehnte sie zuerst ab, gab aber doch nach. Ich fühlte mich erleichtert. Wir verabredeten, uns bei der Großtante zu treffen.

Diese Zusammenkunft bei der Großtante war der Anfang einer langen Reihe von schönen gemeinsamen Stunden an geheimen Orten, sogar in den stinkenden engen Gassen, die mit Moskitos verseucht sind. Als ich wieder in die Schule ging, vernahm ich von meinen europäischen Mitschülern, wie sie ihre Freundinnen in deren Elternhäusern besuchten und sie sogar ins Kino und auf Parties mitnehmen durften. Ich aber wagte das noch nicht, denn es war uns Afrikanern fremd.

Obwohl es bei uns Afrikanern nicht üblich ist, konnte ich Lila nach einer langen Auseinandersetzung überreden, mich ihren Eltern vorzustellen und um Erlaubnis zu bitten, dass wir beide tanzen gehen dürfen. Ihre Mutter, eine etwa 35jährige Frau, war anfangs bestürzt, als sie mein Vorhaben vernahm.

„Na dansi yenyewe iko wapi?” aliniuliza.

„Iko Sauni mama,” nikamjibu kwa adabu.

Sauni ni kiunga cha mji wa Mombasa; na hii inamaanisha kuwa, ikiwa atatoa idhini, basi atakuwa amekubali kwamba malazi pia yatakuwa huko huko baada ya rumba. Sijui kama wazo hili lilimkera au la. Ikiwa lilimkera, basi hakuonyesha kwa kufuatia swali aliliniuliza, „Na ya pesa?”

„La mama, ni ya harusi.“

„Haya, nendeni. Lakini pole pole ni ... Na angalieni walevi,“ akatuonya. (Uk. 27).

Es war eine Hochzeitsfeier, an der jeder mit oder ohne Einladung teilnehmen konnte. Das Tanzlokal war gesteckt voll von Menschen verschiedener Herkunft – auch Besoffenen, Dieben und Prostituierten dabei - und verschiedenen Alters. Sie hatten nur das eine gemeinsam: sie alle wollten sich unterhalten. Auf einmal kam eine Frau auf Lila zu und begrüßte sie. Lila war sehr verlegen, denn es war ihre Taufpatin. Diese erkundigte sich nach Lilas Tanzpartner. Ich wurde ihr vorgestellt.

Alimdadisi Lila kwa muda na mwisho akamwuliza kwa sauti ya chini, „Kwani yu dini gani?“ Ingawa alinijua dini yangu, nadhani hakutaka kumpa mama wa ubatizo nafasi ya kunichambua zaidi. Kwa hivyo alinigeukia akaniuliza, „Ati wewe u dini gani?“

„Mimi ni Mkristo,“ nikajibu.

Ukweli ni kwamba jibu hili halikumtoshwa mamake. Yeye alikuwa akitaka kunisikia nikisema kuwa ni Mkatoliki au mfuasi wa mojawapo ya madhehebu ya Kiprotestanti. (...)

„Haya kwa herini, na sitaki aibu Lila,“ alionya kwa sauti. (Uk. 28-29).

Wir gingen tanzen. Wir tanzten bis in der Früh. Ich schlug vor, daß wir in die „Wohnung“ meines „Bruders“, der auch im Tanzlokal war, schlafen gehen sollten. Sie stimmte sehr zögernd zu. Als ich bei ihm anklopfte, war er überrascht, daß ich ein Mädchen bei mir habe. Er ging hinein und sprach leise mit einer Frau, die bei ihm war. Da es im Haus kein Licht gab, mussten sie ihre Kleider mühsam zusammensuchen. Als die Frau mich sah, war sie verlegen. Danach verschwanden sie eilig.

Es war heiß in dem Haus, das weder eine Lampe noch ein Fenster hatte. Wir tasteten im Dunkeln, bis wir das Bett fanden. Lila und ich zogen unsere Schuhe aus und gingen zu Bett. Ohne auch nur eine Weile zu verlieren, drehte ich mich zu Lila hin. Als sie merkte, was ich vorhatte, begann sie zu weinen.

„Nini sasa?“ nikamuuliza.

„Mimi nimekweleza kila kitu, lakini wewe huniamini bado (...) Umenileta huku utimize haja zako (...) Haya endelea (...)“ Alisema haya kwa sauti ya kusikitisha sana na huku akilia.

„Maskini msichana wa watu,“ nikawaza.

Ningeendelea kwani hakunishika wala kunizuia asilan, lakini moyo wangu uliguswa. Nilijiinua nikalala kitandani – nguvu zote zikawa zimetoweka – ‘moto’ ukawa umenitoka na mwishowe nikajiona mkosa adabu.

„Kumradhi basi, eee Lila?“ nikaanza kumbembeleza. „Sitakufanyia chochote usichokitaka (...) Niamini tafadhali,“ nikamsihi.

Alijibu kwa kuutia uso wake kifuani mwangu akalia kwa chechevu mpaka machozi yake yakalowesha shati yangu. Sikuwa na la kusema wala kufanya, ila nilikaa kimya nikingojea anyamaze. Nisingejali kulia kwake ningeliendelea, kama wengi wafanyavyo, tena bila wasiwasi. Lakini kulia kwake kulinifanya niujiulize madhumuni ya mapenzi ni nini. Ni kufurahisha mtu mmoja ama wawili wanaohusika? (Uk. 31-32).

Als ich mitten in der Nacht aufwachte, spürte ich Moskitobisse auf meinen Wangen. Das Haus war voll von diesen Insekten. Es sind jene Moskitos, die leise fliegen. Man merkt nicht, wann sie sich einem nähern. Am meisten hatte Lila darunter gelitten, denn ihr Gesicht, ihre Hände und ihre Beine lagen frei. Ich schaute mich um. Es war kein ordentliches Haus, sondern eine Hütte mit einem Sandboden und einem Grasdach.

In der Früh beeilten wir uns, nach Hause zu kommen, denn es war Sonntag und für Lila der Tag, in die Schule zurückzukehren. Da sie ihre Wäsche schon gewaschen und gebügelt hatte, konnte sie ohne Verzögerung alles schnell einpacken.

Lilas Mutter wartete auf uns. Während ich in der Stube saß, kochte Lila das Mittagessen für uns. Nach dem Essen half ich ihr einpacken. Sie verabschiedete sich von Bekannten und Verwandten, zog ihre Schuluniform an und ging mit mir zum Bahnhof, wo es von Eltern, Geschwistern und Freunden wimmelte, die gekommen waren, sich von den Schülern und Schülerinnen zu verabschieden. Lila versteckte ihre Gefühle mir gegenüber, die sie in der Öffentlichkeit nicht zeigen wollte. Sie verabschiedete sich ruhig und verhalten.

Ich fühlte mich ohne Lila sehr einsam. Vier Tage nach ihrer Abreise erhielt ich einen Brief von ihr, der Freude in mein Herz brachte. Ich antwortete gleich, denn auch meine Schulferien gingen zu Ende. Wir schrieben einander öfters und erfuhren langsam, was Liebe eigentlich ist.

Sie kam in mein Heimatdorf zu den Weihnachtsferien. Es wurden aufregende Tage. Wir hatten drei Anlässe zu feiern: Uhuru¹⁶, Weihnachten und Neujahr. Für die Jugend war es eine günstige Gelegenheit, sich zu unterhalten und neue Freundschaften anzuknüpfen. Lila hatte meiner Einladung, bei uns im Dorf Beri Weihnachten zu verbringen, zugestimmt und ihre Mutter hatte es ihr gestattet. Die Frage, die Lila mir aber stellte: „Niende kama nani?“ (uk. 46) ließ ich unbeantwortet. Damit es im Dorf nicht auffalle, schlug ich vor, dass jeder für sich allein dorthin fahren sollte, zuerst ich und später sie.

Kwa kulingana na sheria za kimila sikuwa na uwezo wa kumwalika msichana yeyote kwetu. Hatuna neno linaloeleza ushusiano kati ya msichana na mvulana kabla ya uchumba. Ni kawaida ya mtu kuwa na mpenzi, lakini ni marufuku na hathubutu kumleta kwao kabla ya ndoa. Na wasichana nao jadi yao ilikuwa kutojionyesha hadharani na yule ampendaye kabla ya uchumba; na hata baada ya posa, wachumba hawakutakiwa kuonekana pamoja ovyo ovyo. Na ikiwa mambo yalikuwa hivi, itakuwaje basi msichana aonyeshe mapenzi yake kwa mvulana na hata awe na ujasiri wa kuzuru kwao? Kwa hivyo Lila hakuwa na kibali chochote kwetu – aje kama nani? (Uk. 49)

Ich fuhr mit dem Bus, genannt Mwanamwali (Jungfrau), am folgenden Tag sollte Lila folgen.

Die Fahrt war ermüdend, da die Straße im schlechten Zustand war. Die großen Löcher und der Staub machte uns allen zu schaffen. Die Landschaft mit den Maisfeldern war aber schön. Mein Heimatdorf Beri ist zwar klein, aber wohlhabend und weithin

¹⁶ Nationalfeiertag

bekannt. Es gibt dort zwei Geschäfte, ein Restaurant, wo Tee und maandazi (Pfannkuchen) serviert und Obst verkauft wird. Eine breite Straße führt durch das Dorf.

Wir sind eine große Familie mit vielen Verwandten. Alle Frauen und Mädchen waren damit beschäftigt, für das Fest zu kochen. Im Saal, wo mein Großvater saß, waren viele Familienmitglieder versammelt, denen er gute Ratschläge gab. Bei solchen Anlässen wurden die gegenwärtige Lage und die weitere Entwicklung der ganzen Familie besprochen.

Meine Schwester Zime ging inzwischen zur Bushaltestelle, Lila abzuholen, die dann der Familie vorgestellt wurde. Meine Geschwister Feni, Tina und Dina waren auch da. Die Anwesenden merkten, dass ich Lila zwar umarmen wollte, aber mich nicht traute, dies in der Öffentlichkeit zu tun. Ich hatte sie mit gemischten Gefühlen erwartet, denn ich konnte im voraus einschätzen, wie meine Familie sie aufnehmen würde. Ich stellte Lila meinem Vater und meiner Mutter vor und danach meinem Großvater.

Kwa moyo mzito nilimpeleka ili nimjulisha kwa babu. Hofu iliniingia nikaanza kujilaumu kwa nini kujitia kwenye ujasiri nisiuweza? Mawazo ya babu juu ya urafiki kati ya msichana na mvulana walio wanafunzi hayakuwa mageni kwangu. (...) ... babu aliinuka na kutulaki kwa mikono miwili! (...)

„N’ nani huyu Matano?“ aliniuliza kwa uso wa furaha.

„Aitwa Lila ... Tede Lila. Ameku-“

„Rafiki yako sio?“ akaniingilia kati.

„Ndiyo Babu,“ nilijibu na kiwewe.

„Oo, vyema sana. Kwa hivyo kumbe ni mke wangu!“ Na hapo alimshika mkono akamkumbatia kwa furaha. Lila naye hakutaka kushindwa; kwa uso mkunjufu akasema, „Iii, lakini bado hajanioa!“

„Hiyo siyo kitu. Wewe mradi ushafika nyumbani juwa (jua) u mke wangu, (...). “Haya nyanya, karibu nyumbani kwetu ambako ni kwenu tokea leo.” (Uk. 68- 69).

Ich musste staunen, dass mein Großvater, der sonst so streng war, Lilas Besuch zugestimmt hatte. Lila verbrachte schöne Festtage bei uns. Wir waren bei der Christmette, bei Familientreffen und bei Tanzveranstaltungen beisammen.

Schon drei Jahre waren wir Freunde. Es verging keine Woche, ohne daß wir wenigstens für kurze Zeit beisammen waren. Die erste Trennung war für mich auch der erste Prüfstein. Beim Abschied verlangte sie von mir, dass ich ihr treu bleibe.

„Apa, hutanisahau Maa..taa..noo..“ aliniuliza na kuniomba kwa sauti dhaifu na ya kufifia.

„Naapa,“ nami nilijibu nikiwa katika hali ile ile dhaifu.

„Apa hutajishughulisha na wengine.“

„Naapa.“

„Apa, ufikapo tu, utaniandikia.“

„Naahidi na kuapa pamoja; (...)?“ (Uk. 72).

Ich verabschiedete mich von ihr und fuhr in die Stadt, wo ich mit meinem Studium an der Universität begann. Das Leben dort war sehr aufregend, da alles für mich neu war.

Niliyakuta maisha ya Chuo Kikuu ni ya kuvutia na kuisimua kabisa. Akina dada walikuwa wa kuvutia macho na kuchemsha damu, hasa kwa mwanfunzi mgeni kama mimi. Hali kama hii ya ugeni ilitufanya wengi wetu tusaliti mapenzi yetu kwa wale tuliowaacha nyuma; si waume si wake, wengi walisahau wapenzi wao siku chache tu baada ya kutia mguu Chuo Kikuu. (Uk. 78)

Ich ließ mich aber von diesem Strom nicht wegtragen, denn die Liebe zu Lila gab mir die Kraft durchzuhalten. Als ich im dritten Jahr war, hatte Lila die Form IV der Sekundarschule beendet und bekam Gelegenheit, eine Ausbildung in der Stadt anzutreten.

Einige Tage nach ihrer Abreise erhielt ich einen Brief von ihr, worin sie mir mitteilte, daß sie gut angekommen sei und der Unterricht bereits angefangen habe. Wir schrieben einander Briefe und unsere Liebe half mir, fleißig zu studieren. Wir hatten schon beschlossen, den Lebensweg gemeinsam zu gehen und unsere Eltern hatten uns bereits den Segen¹⁷ gegeben. Offen blieb nur noch der Zeitpunkt.

Auf einmal geschah etwas, das ich mir nie zu denken getraut hätte. “ (...) giza lilingia maishani mwangu bila ya hodi” (uk. 87). Lila schrieb mir keine Briefe mehr.

Als sie einmal in den Ferien daheim war, staunte ich über das teure und schöne Kleid, das sie trug.

„Unalipenda?“

„Sana.“

„Nilipewa ni...“

„Nani?“ nikamkatia na huku shaka ikiniingia moyoni.

Alifafanua nafsi yangu akaonelea afadhali anieleze kwa kirefu. „Wajua,“ akaanza, „kule shule kuna mwalimu mmoja wa kike ambaye tunapatana sana. Sasa, siku moja alikwenda kwao Ulaya akanunua hili rinda. Lakini kwa kuwa ananenepa kwa haraka sana, hakulivaa kwa muda mrefu kwani halikumwingia, na ...“

„Ndipo akakupa?“

„Ehe.“

„Yanaonekana anakupenda sana.“

“Nimekuambia ni rafiki yangu,” akakaza.

Ilinibidi nikubali. (Uk. 88-89).

Mir war es jetzt schon klar, dass sie nicht mehr die Lila von früher war. Die Osterferien gingen zu Ende und wir verabschiedeten uns neuerlich.

Ich schrieb ihr einen Brief sofort nach meiner Ankunft an der Universität, aber fast zwei Monate lang erhielt ich keine Antwort. Den Brief den sie mir dann schrieb war unpersönlich und kalt. Ich schrieb ihr mehrere Briefe, aber sie ließ nichts mehr von sich hören. Als ich während der Ferien wieder nach Hause zurückkehrte, erkundigte ich mich nach ihr. Ich erfuhr, daß sie bei der Taufpatin in Majengo weilte. Ich eilte dorthin. Lilas Taufpatin erkannte sofort meine innere Verfassung.

¹⁷ “(...) kutupa radhi“ (uk.. 86)

“Karibu baba,” alitangulia kusema.
„Asanteni.“ Na huku nikisongea, „Shikamoo ...“
„Marahaba ...“
„Poleni kwa kuwaingilia mapema hivi,“ nilianza kwa kuomba msamaha.
„Hapana neno, Baba,“ akaanza kuniridhisha. “Kwanza ni baraka kupata mgeni asubuhi. Felix,” akaita. “Hebu lete kiti hapa.”
Felix alileta kiti, na mama akanikaribisha. “Karibu ukae, Baba.” Akamgeukia Felix, “Nenda umwambie Lila kuna mgeni wake.”
Nilikaa. Kwa hakika sikujua kama uso wangu ulionyesha furaha au huzuni ingawa kusema kweli akili yangu ilikuwa imepooza. Huyu mama yamkini alinitambua hali yangu, akaonelea anizungumzishe.
“Habari ya safari, Baba?”
“Njema tu. ... Habari za siku nyingi?” nikawahi kuongezea.
„Tunashukuru, hatuna neno. Habari za masomo?”
“Ninaendelea vyema.”
„Vizuri. Umewasili lini?”
„Leo alfa...”
„Kwa hivyo hujapumzika!”
„Bado; lakini sikuchoka sana. Si tumelala basini?”
“Hata hivyo, safari ni safari.” Aliangalia ndani na akapaaza sauti, „Wewe Lila, husikii mwenzako amekuja?”
“Naja,” lilikuja jibu la kinyonge.

Jibu hili la kinyonge lilivunja moyo wangu kabisa. Siye Lila niliyekuwa nikimjua. Niliyekuwa nikimjua harufu yangu tu ilimtosha kumtoa mbio mahali popote alipokuwapo, kama nyoka atokavyo pangoni maji ya moto yatiwapo. Huyu wa leo, kutokana na kauli yake, alikuwa hataki kuniona! Nilisinyaa.

Lila alitoka kinyonge, na aliponiona akajitia kushtuka.
„Ala! Kumbe ni wewe! Hujambo?” na huku akinyoshea mkono.
„Sijambo,” nilimjibu huku nikiushika mkono wake ambao, kwa kuwa alikuwa akitoka kuoga, ulikuwa baridi mithali ya uhusiano wetu ulivyokuwa kwa wakati ule.
„Karibu. ... Karibu, ndani,” akanikaribisha.
„Ingia ndani, Baba,” mama akasisitiza. “Mpikie chai basi mwenzako,” Lila akahimizwa.

Nilimtupia jicho¹⁸ Lila. Alionekana mnyonge, amekonda na mwenye ujasiri wa kujipa. Nadhani alikuwa akiungojea mkutano huu wetu kwa woga na huzuni pamoja. Nadhani kwamba angeweza, angeahirisha kukutana kwetu milele. Lakini kwa sasa, kwa kuwa nilikuwa nimemkuta kwa ghafula, hakuwa na la kufanya. Ilimbidi ajifanye hajali. (Uk. 93-94).

*Ich dachte mir: (...) mbele hakuendeki na nyuma hakurudiki*¹⁹. Lililosalia lilikuwa yeye kutapatapa. (Uk. 94).

Ich trank ein wenig Tee. Lila und ich saßen einander zunächst wortlos gegenüber. Langsam kam aber doch ein Gespräch zustande.

¹⁸ Redewendung

¹⁹ Redewendung

“Habari za masomo?”
 “Nzuri tu,” alijibu kwa mkato na wala hakunirejeshea kama ilivyokuwa kawaida yake.
 “Mlifunga shule lini?”
 “Juzi juzi tu.”
 “Kwa nini hukuniandikia na kuniarifu?”
 “Nilisahau.”
 “Tokea lini usahaulifu huo?”
 “Sijui.”
 “Lila, mbona hivi?” Nilimuuliza na nikaongezea, „Kitu gani kinachokuzuzua?“
 „Sina,“ alijibu kwa ukaidi.
 “Huna! Kwa hivyo mambo kama kawaida; si ndivyo?”
 “Sio.”
 “Kwa nini?”
 Kimya.
 “Kwa nini?” nikarudia swali.
 “Wewe nawe, unadadisi hivyo kama ...”
 “Hujanijibu bado,” nikasisitiza.
 “Wataka jibu?”
 “Tena haraka sana.”
 “Sitaki tena; si basi,” akajibu kwa ufedhuli na ukatili mumo humo.
 Aliposema haya, hasira zilinipanda nikamjibu, “usiwe mjinga ... Unadanganywa na ulimwengu, dada ...”
 “Sijali. *I know what I am doing*. Si mtoto tena,“ akafoka. (Uk. 95-96).

Ich versuchte herauszufinden, was ich falsch gemacht, worin ich gefehlt hatte.

„Hukunifanyia chochote ; lakini sijisikii tu basi,“ alisisitiza.
 „Haiwezekani. ... Yaani uliamka usiku mmoja na ukajisikia hunipendi tena?“
 Hakujibu.
 Nikaendelea, „Usinifiche tafadhali. Niombacho ni kuambiwa wazi. Ikiwa nimekukosea, sema. Ama ikiwa sina kasoro yoyote, basi naona kisa cha baa hili ni mvulana mwenzangu tu! Nini kunificha?“
 “Si mvulana!” akakana.
 “Ni mvulana!” nikakaza.
 “Haya basi ni mvulana; wataka nini?”
 “Wewe,” nikasema kijinga.
 “Sikutaki! Husikii?” akipandwa na hasira.
 „Wacha ushe ...“
 „Mshenzi na wewe pia,“ akamaliza.
 “Si kitu; lakini fahamu unajidanganya. ... Kitu ni kwamba ungali wanipenda lakini sasa sema umepatwa na mkosi fulani. Ikiwa ndivyo, niko tayari kukusaidia na kukusamehe ili tuanze upya. Tayari?”
 “Sikupatwa na mkosi wowote; kitu ni kwamba sijisikii tu. Husikii?”
 “Fikiria mamako, asikiapo ...”
 “Hana neno. ... Hajala mahari ya mtu bado,” akanikata.
 „Fikiria wazazi wangu ... wakisikia tumeachana ...?
 „Sasa sijisikii; nijilazimishe?“
 „Fikiria rafiki zetu – watasemaje?“
 „Wacha waseme!“
 „Jifikirie.“

„Liwalo na liwe²⁰, mimi sijali.“ (Uk. 96-97).

Jeder Versuch, mit ihr zu sprechen, wurde abrupt zurückgewiesen. Schließlich forderte sie mich auf, mir ein anderes Mädchen zu suchen.

„ (...) Nakuomba uje upate msichana mwingine ambaye atastahili mapenzi yako kuliko mimi nilivyokufanyia na kukuachia ukiwa hali bado ni hai.“ „Sahau,“ nikasema, „juu ya mimi kupata msichana mwingine kukuzidi. Wasichana ni mahamri ambayo mtu aweza kwenda akachagua na kununua. Kupata msichana si jambo rahisi, na hasa kupata msichana kukuzidi wewe najua sitapata. ... Sikiza (sikiliza) Lila, nafahamu tu kwamba yuko anayekuzuzua, nami najua hofu na kiziwi kwa yote yaliyokuwa ya thamani na azizi kwetu. Niko radhi kukusamehe ili tuanze upya. Nakuomba Lila, fikiria tena; haya!”

Alipoona majadiliano yanazidi alisema, “Aaa, wewe nawe! Ni kunisumbua tu! Nimeshakwambia kila kitu, husikii? Haya basi, ni shauri yako sasa.” Na hapa aliinuka na kuondoka. (uk. 97-98).

Sie stand auf, ging auf ihr Zimmer und verschloß die Türe. Ich fragte mich: Ilikuwa nimlaumu nani? Yeye, mimi au ulimwengu. (Uk. 99).

Die folgenden Tage waren für mich leer und sinnlos, bis ein Freund - Ngilo hieß er - mich besuchte und mich einlud, mit ihm spazieren zu gehen. Zufällig trafen wir dabei Lila. (...) lakini nilijikaza kisabuni kwa kupishana naye bila ya hata jambo. Naye alifanya vivyo hivyo kwani sote hatukuweza kuficha hali yetu ya upweke (...) (Uk. 100).

Ich besuchte Lilas Mutter. Wir sprachen lange miteinander über diese Wende. Auch sie konnte sich diesen plötzlichen Abbruch nicht erklären.

„Mtoto huyu amerogwa (amelogwa) bila shaka,“ mamake alidokeza nilipomwendea kumwarifu kwisha kwa urafiki wa binti yake na mimi.

„Huenda ikawa,“ nilimtia moyo kwani hangekubali kwa mwanawe amenaswa na maisha ya anasa ambayo hawezi kujitoa tena.

„Basi, baba, wewe usife moyo. Mimi nitampeleka kwa Kajiwe.”

“Ikiwa atakubali.”

Nilisema hivi kwa kuwa toka tugombane, Lila alianza tabia ya kutomsikiza hata mamake. Alikuwa ametupiwa ndumba kweli nini? (uk. 101).

Ich kehrte zur Universität zurück. Ich hatte Lila bereits aus meinem Gedächtnis gelöscht und konzentrierte mich ganz auf das Studium.

Mwishoni mwa mwezi wa tatu, dunia yangu ikaanza kuingia nuksi. Habari zilinifikia kwamba Lila alikuwa mahuti hospitali; na siku chache baadaye, nilipokuwa naenda kula chakula cha mchana, nikapokea simu ya upepo yenye habari za kifo chake!

Hapa nakuachia wewe msomaji²¹.

²⁰ Redewendung

²¹ So wie es in der Oralliteratur üblich ist, verabschiedet sich der Ich-Erzähler von seinen Hörern bzw. vom Leser.

Woran sie starb, blieb eine offene Frage. Von sich selbst sagte der Ich-Erzähler: (...) nikaanza kulia. (Uk. 102).

Tamati